# USTAHIMILIVU WA TABIANCHI

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

FOSTA HEALTH

GCRFAFRICAP
CLIMATE SMART AGRICULTURAL DEVELOPMENT

Centre for Climate Change Economics and Policy
An ESRC Research Centre

MRADI ULIYOFANYWA NA CCCEP | MUHTASARI NAMBA 1 | SEPTEMBA 2024



## USTAHIMILIVU WA TABIANCHI?

Katika enzi ya kuongezeka mifumo ya tabianchi isiyotabirika, ni muhimu kwa jamii, na mtu mmoja mmoja kuanza kujiandaa, kukabilina ili kuepukana na athari mbaya za mabadilko ya tabianchi. Hii inasisitiza umuhimu wa kutengeneza mifumo ya kuwezesha kustahimili mabadiliko ya tabianchi.

Uhimilivu wa tabianchi unahusu uwezo wa mifumo ya kijamii, kiuchumi, na kimazingira kukabiliana na matukio, mwendendo, au misukosuko inayohusiana na tabianchi.

Wakati serikali na wadau wa maendeleo wamewekeza katika kuimarisha uhimilivu wa jamii na mandhari, kunahitaji miongozo na juhudi mbalimbali kufanikisha lengo hili. Changamoto katika kuelewa dhana ya uhimilivu, ukosefu wa mifumo sahihi na viashiria vya uhimilivu, pamoja na rasilimali chache za kifedha na kiufundi, vyote vinazuia wataalamu kutekeleza na kutathmini juhudi za kujenga uhimilivu.

### USTAHIMILIVU WA VYANZO MBALIMBALI VYA KUJIKIMU

Katika muktadha wa miradi ya maendeleo, ni muhimu sana kuzingatia miradi ya kujikimu inayo saidia watu kuhistamili tabianchi. Mbinu hii haipunguzi tu umasikini na kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko, bali pia hutumika kama kiashiria muhimu cha mafanikio ya mradi.

Vyanzo mbalimbali vya kujikimu vyenye ustahimilivu vinanaweza kudumishwa na kuboreshwa kaika maisha ya wanajamii shughuli zao za kila siku hata kipindi cha mabadiliko, ikiwa ni pamoja na kukabili mishtuko na misukosuko mbalimbali. Jamii inaweza kujilinda dhidi ya changamoto hizi kwa kutumia uwezo wa rasilimali na mali walizo nazo, kwa kufanya kazi kwa pamoja, kushirikiana na kutumia mitandao mbalimbali na kujifunza kutoka kwenye miradi mbalimbali ya majaribio, changamoto na fursa zilizopo. Kusaidia kuimarisha uhimilivu wa maisha ni jambo la msingi katika kujenga mandhari na jamii zenye uhimilivu wa tabianchi.

Watafiti wa Chuo Kikuu cha Leeds walitumia mfumo wa uhimilivu wa maisha ya kujikimu kutathmini athari za mradi wa ujumuishaji wa mabadiliko ya tabianchi uliotekelezwa Kaskazini mwa Tanzania.

### KUJENGA UHIMILIVU WA TABIANCHI WENYE UFANISI

**1** Katika juhudi za uhimilivu ni muhimu kuzingatia watu na jinsi ya kujikimu na maisha.

**2** Inatambua kwamba mifumo ya kijamii na kimazingira inauhusiano, lakini pia inakabiliwa na changamoto za kimaamuzi.

**3** Unafanya mradi kuwa na athari chanya endelevu na hata mradi kuisha muda wa utekelezaji

#### Mfumo wa Uhimilivu wa Maisha ya Kujikimu (Speranza et al. 2014)


**Uwezo wa Kuzuia Athari** – Hii inahusu "uwezo wa kupunguza athari za mabadiliko na kutumia fursa zinazojitokeza ili kufanikisha matokeo bora ya maisha " inajumuisha aseti au mitaji (mtaji wa kibinadamu, mtaji wa mali za asili, mtaji wa kijamii, mtaji wa kifedha na miundombinu).

**Uwezo wa Kujimudu Kujiendasha/Kujitegemea** – Hii inahusu uwezo wa kijamii kuamua kanuni zao wenyewe zinazowaongoza katika ushirikiano wa kijamii. Hali hii inaweza kufanikishwa kwa njia zifuatazo: kuunda mitandao ya kijamii, kuimarisha ushirikiano na kuongeza idadi ya watu wengi wanaojitegemea.

**Uwezo wa Kujifunza** – Hii inahusu uwezo  wa kijamii kupata maarifa na ujuzi mpya pamoja na uwezo wa kuyatumia kwa vitendo. Maarifa mapya yanapaswa kusaidiwa ili yahame  kutoka nadharia kuwa ya vitendo.

## MPANGO JUMUISHI WA KUJENGA UHIMILIVU WA TABIANCHI: UTAFITI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ili kukuza uelewa wa muktadha wa viashiria muhimu vya uhimilivu wa maisha na kutathmini mabadiliko ya viashiria hivi kwa muda, utafiti uliofanywa kwa kulinganisha kaya zilizoshiriki na zisizoshiriki kwenye mradi katika eneo la Milima ya Usambara Mashariki umewezesha watafiti na wataalamu kupata uelewa wa kina kuhusu juhudi za kujenga uhimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.




Athari chanya kwenye viashiria muhimu vya uhimilivu (zilizoangaziwa kwa rangi ya kijani) nionaonyesha matumaini. Uwezo wa kujifunza uliimarishwa kupitia vyanzo mbalimbali vya taarifa, kuanzishwa kwa majukwaa ya majaribio ya kilimo hifadhi, kukuza elimu ya kifedha na ujasiriamali. Kujiandaa kwa kujitegemea kulihamasishwa kupitia shughuli za vikundi na upanuzi wa mitandao ya kijamii (angalia Muhtasari namba 4).

Hata hivyo, shughuli za msingi zilizolenga kuimarisha uwezo wa kaya kujihimili, kama vile miradi ya kuongeza kipato (mfano, ufugaji wa vipepeo, utalii wa ikolojia), ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, na upanuzi wa masoko mapya, zilionyesha athari ndogo za mradi (zilizoangaziwa kwa rangi nyekundu). Kwa hivyo, juhudi za ziada zinahitajika ili kuhakikisha kuwa maarifa na mafunzo yaliyotolewa yanaimarisha uwezo wa msingi unaohitajika na kufanikisha malengo ya mradi kwa kuyageuza kuwa vitendo.

### MAFUNZO YALIYOPATIKANA

- Kujikita katika kujifunza na kujaribu mambo mapya kunachangia katika kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko, lakini hakuhakikishi kwamba maarifa yatatafsiriwa kwa vitendo.
- Kujengea maarifa kwa vitendo unahitaji miradi ya muda mrefu na kujitolea kwa muda mrefu.
- Vikundi vinasaidia mitandao na kujiandaa kwa kujitegemea, lakini juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha ushirikiano na kutathmini ufanisi wa vikundi.
- Uelewa wa viashiria muhimu vya uhimilivu wa maisha ya kujikimu unahamasisha majukumu ya pamoja kwa ajili ya uhimilivu wa hali ya hewa, lakini ukosefu wa rasilimali unaweza kudhoofisha uendelevu.

## MAPENDEKEZO

- Lenga katika kuimarisha uhimilivu wa maisha ya kujikimu ili kusaidia malengo ya uhimilivu wa mabadiliko ya Tabianchi na kupunguza umaskini kwa wakati mmoja.
- Tengeneza mbinu za utekelezaji kwa kuzingatia uelewa wa kina. Pia kuongeza muda wa mradi ili kuhakikisha maarifa yanatolewa yanatafsiriwa kwa vitendo.
- Fanya tathmini ya mara kwa mara ya mienendo ya vikundi ili kuhakikisha ushirikiano wenye ufanisi na uendelevu, wakati wa utekelezaji wa mradi na hata baada ya kukamilika kwake.





Prepared and disseminated through collaboration with the ESRC Climate Change Centre for Economics and Policy Legacy project led by UoLeeds and Tanzania Forest Conservation Group

To find out more about the project, please visit fosta-health.eu